# KUWEPO KWA MOLA MTAKATIFU NO. 2

<"xml encoding="UTF-8?>

BISMILAHI RAHMANI RAHIYMI

KWA JINA LA MWENYEEZI MUNGU MWINGI WA REHEMA MWENYE KUREHEMU

KUWEPO KWA MOLA MTAKATIFU NO.2

Sisi tunaamini kuwa Mwenyeezi Mungu ndiye muumbaji wa vitu vyote, na athari ya utukufu na elimu yake inaonekana kwa uwazi kabisa katika kila kiumbe ulimwenguni, katika umbile la .mwanaadamu, wanyama, mimea, katika nyota ziliopo mbinguni, na katika kila kitu ulimwenguni

Sisi tuna itikadi ya kuwa; kila tukifikiri na kutafakuri zaidi kuhusiana na siri ya viumbe vyote duniani, tutafahamu utukufu wa elimu na qudra ya dhati ya Mola Mtakatifu, na kwa kuonekana maendeleo ya elimu na taaluma ya wanaadamu ya kila siku kunapatikana na kufunguka elimu mpya kutokana na elimu na hekima zake Allah (s.w), na tafakuri za wanaadamu zinazidi kukua na kuenea kwa wingi zaidi, na tafakuri hizo ndio chanzo cha kuwa karibu naye Mola mtakatifu .na kunufaika na upeo wa nuru ya utukufu wake

DHATI YA ALLAH (S.W) IMETAKASIKANA ISIYOKUWA NA MWISHO. .3

Sisi tunaamini kuwa dhati ya Mwenyeezi Mungu imeenea sehemu zote, naye hana mwanzo wala mwisho, dhati hiyo inaonekana katika elimu yake, qudra ya utukufu wake, kubakia kwake milele katika sehemu zote na zama zote, na kwa sababu hiyo basi ndio tukasema kuwa Mwenyeezi Mungu hana sehemu maalumu wala kipindi maalumu, kwa sababu sehemu au nafasi na zama zina kiwango maalumu, ijapokuwa Mwenyeezi Mungu hana sehemu maalumu wala zama maalumu lakini Yeye yuko katika sehemu na zama zote, kwa sababu dhati ya -:utukufu wake ni iko juu zaidi kuliko sehemu na zama, kama tunavyosoma ndani ya Qur-ani

وَهُوَ الَّذِى فِى السَّمَاء إِلَهٌ وَفِى الاَرْضِ إِلَهٌ وَهُوَ الْحَكِيمُ الْعَلِيمُ[1]

Na Yeye ndiye Mungu mbinguni, na ndiye Mungu katika ardhi. Naye ndiye Mwenye hikima, .Mwenye ujuzi

هُوَ الَّذِى خَلَقَ السَّمَاوَاتِ وَالاَرْضَ فِى سِتَّةِ اَيَّامٍ ثُمَّ اسْتَوَي عَلـَي الْعَرْشِ يَعْلَمُ مَا يَلِجُ فِى الاَرْضِ وَمَا يَخْرُجُ مِنْهَا وَمَا يَنزِلُ مِنَ السَّمَاء وَمَا يَعْرُجُ فِيهَا وَهُوَ مَعَكُمْ اَيْنَ مَا كُنتُمْ وَاللهُ بِمَا تَعْمَلُونَ بَصِيرٌ[2]

Yeye ndiye aliye ziumba mbingu na ardhi katika siku sita; kisha akakaa vyema juu ya enzi. Anayajua yanayo ingia katika ardhi na yanayo toka humo, na yanayo teremka kutoka mbinguni,

na yanayo panda humo. Naye yu pamoja nanyi popote mlipo. Na Mwenyezi Mungu ni Mwenye .kuyaona mnayo yatenda

Ndio, Mwenyeezi Mungu yuko karibu na wanaadamu, na Mwenyeezi Mungu yuko ndani ya nafsi za wanaadamu, Naye yuko katika sehemu zote, hali ya kwamba hana sehemu, makani, .wala zama maalumu

وَلَقَدْ خَلَقْنَا الإِنسَانَ وَنَعْلَمُ مَا تُوَسْوِسُ بِهِ نَفْسُهُ وَنَحْنُ اَقْرَبُ إِلَيْهِ مِنْ حَبْلِ الْوَرِيدِ[3]
Na hakika tumemuumba mtu, nasi tunayajua yanayo mpitikia katika nafsi yake. Na Sisi tuko karibu naye kuliko mshipa wa shingoni mwake.
Maelezo yanayopatikana katika Aya hiyo.
.Aya hiyo inataja ujuzi wa Mwenyeezi Mungu na uweza wake

هُوَ الاَوَّلُ وَالآخِرُ وَالظَّاهِرُ وَالْبَاطِنُ وَهُوَ بِكُلِّ شَيْءٍ عَلِيمٌ[4]

Yeye ndiye wa Mwanzo na ndiye wa Mwisho, naye ndiye wa Dhaahiri na wa Siri, naye ndiye Mjuzi wa kila kitu.
-:Kwa hiyo, ikiwa katika Qur-ani tunasoma

ذُو الْعَرْشِ الْمَجِيدُ[5]

Mwenye Kiti cha Enzi, Mtukufu,Neno “ARSHI” lililokuja katika Aya hiyo halimaanishi kiti cha ufalme, bali linamaanisha utukufu na mamlaka yake Allah (s.w), na ikiwa katika Qur-ani :tunasoma

[6]الرحمن علي العرش استوي

ARRAHMANI ALAL_ARSHI STAWAA""
Aya hiyo haina maana ya kuwa; Mwenyeezi Mungu ana sehemu au zama maalumu, bali inathibitisha utukufu wa utawala wake katika ulimwengu mzima wa kimada na ule usiokuwa wa kimada,kwa sababu kama tukijaalia kuwa Mwenyeezi Mungu sehemu au zama maalumu, tutakuwa tumemuweka Mwenyeezi Mungu katika mipaka maalumu, na tumempa sifa ya viumbe, na tukamfahamu Mwenyeezi Mungu kama tunavyovifahamu vitu vyengine vya -:kikawaida hali ya kwamba Yeye Mwenyewe Mola Mtakatifu anasema
فَاطِرُ السَّمَاوَاتِ وَالاَرْضِ جَعَلَ لَكُم مِّنْ اَنفُسِكُمْ اَزْوَاجاً وَمِنَ الاَنْعَامِ اَزْوَاجاً يَذْرَؤُكُمْ فِيهِ لَيْسَ كَمِثْلِهِ شَيْءٌ وَهُوَ السَّمِيعُ البَصِيرُ[7]
Yeye ndiye Muumba mbingu na ardhi, amekujaalieni mke na mume katika nafsi zenu, na katika

nyama hoa dume na jike, anakuzidishieni namna hii. Hapana kitu kama mfano wake. Naye ni .Mwenye kusikia Mwenye kuona

-:Na katika Aya nyengine anasema

وَلَمْ يَكُن لَّهُ كُفُواً اَحَدٌ[8]

Wala hana anaye fanana naye hata mmoja.
Mungu, Baadhi ya Aya za qur-ani, zinathibitisha kuwa, kiti cha ufalme wa Mwenyeezi Mungu kimeenea mbinguni na ardhini, kwa hiyo, ufalme na mamlaka ya Mwenyeezi Mungu yameenea .ulimwengu mzima, kama tunayosoma katika Suratul-Baqarah Aya ya 255
اللّهُ لاَ إِلَـهَ إِلاَّ هُوَ الْحَيُّ الْقَيُّومُ لاَ تَأْخُذُهُ سِنَةٌ وَلاَ نَوْمٌ لَّهُ مَا فِى السَّمَاوَاتِ وَمَا فِى الاَرْضِ مَن ذَا الَّذِى يَشْفَعُ عِنْدَهُ إِلاَّ بِإِذْنِهِ يَعْلَمُ مَا بَيْنَ اَيْدِيهِمْ وَمَا خَلْفَهُمْ وَلاَ يُحِيطُونَ بِشَيْءٍ مِّنْ عِلْمِهِ إِلاَّ بِمَا شَاء وَسِعَ كُرْسِيُّهُ السَّمَاوَاتِ وَالاَرْضَ وَلاَ يَؤُودُهُ حِفْظُهُمَا وَهُوَ الْعَلِيّ
الْعَظِيمُ
Mwenyezi Mungu - hapana mungu ila Yeye Aliye hai, Msimamia mambo yote milele. Hashikwi na usingizi wala kulala. Ni vyake pekee vyote viliomo mbinguni na duniani. Ni nani huyo awezaye kuombea mbele yake bila ya idhini yake? Anayajua yaliyo mbele yao na yaliyo nyuma yao; wala wao hawajui chochote katika vilio katika ujuzi wake, ila kwa atakalo mwenyewe. Enzi yake imetanda mbinguni na duniani; na wala haemewi na kuvilinda hivyo. Na Yeye ndiye aliye juu, na ndiye Mkuu Maelezo kuhusiana na Aya ya 255 ya Suratul-Baqarah Aya hii huitwa Ayatul-Kursiyyu, aya tukufu kabisa, anahimizwa kila Muislamu kuyaweka maana ya Aya hii mbele ya macho yke daima, ili asimuone muqaddim wala muakhkhir, ila Mwenyewe tu Mwenyeezi Mungu Subhanahu Wataala, na mahala pengi katika hadithi za Mtume amehimizwa mtu kuisoma, kama: a) Baada ya kutoa salamu katika sala, b) kabla ya kulala, c) anapotoka nje, d) anapoingia ndani,
.e) anapokuwa na hofu ya kuogopa vinavyoonekana na visivyoonekana

Surat Az-Zukhruf Aya ya 84 [1]

[2] Surat Al-Hadiyd Aya ya 4

[3] Surat Qaf Aya ya 16

[4] Surat Al-Hadiyd Aya ya 3.

[5] Suratul-Buruj Aya ya 15

[6] Surat Taha Aya ya 5

[7] Surat Ash-Shuura Aya ya 11

[8] Surat At-Tawhiyd Aya ya 4

MWISHO